



Ujumbe wa Muungano wa Ulaya wa Kuangalia Uchaguzi
Jamhuri ya Kenya ó Uchaguzi Mkuu 2013
Tangazo kwa wanahabari: EUEOM/2013/7
Tarehe: 06/03/2013

TANGAZO KWA WANAHABARI

Wakenya wadhihirisha kujitolea kwao kufaulisha uchaguzi wa kidemokrasia

NAIROBI, Tarehe 06 Machi, 2013 – Uchaguzi mkuu wa tarehe 4 Machi, ulikuwa ndio mtihani wa kwanza kwa katiba mpya, msingi mpya wa uchaguzi na vilevile mahakama iliyofanyiwa mageuzi. Ingawa mchakato mzima wa uchaguzi bado haujakamilika, Kenya inaweza kusifiwa kwa kuonyesha msimamo imara kwa uchaguzi wa kidemokrasia. Mchakato mzima wa uchaguzi umeshuhudia kujitolea kidhati kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) na vilevile Wakenya wapiga kura. Ingawa kulikuwa na visa vibaya kadhaa vya vurugu katika baadhi ya maeneo ya nchi, waangalizi wa uchaguzi wa EU wameonelea kwamba, kwa ujumla kulikuwa na utulivu na moyo wa kidemokrasia wa Wakenya ulitawala pakubwa.

Uchaguzi ulisheheni azma kubwa ya wanajamii kuwepo amani, uwazi na kuaminika kwa uchaguzi wenyewe. *“Nilipendezwa sana kuona kujitolea kwa wapiga kura Wakenya ili kutekeleza wajibu wao wa kidemokrasia. Walijitolea kiasi cha kuweza kuhimili hata foleni zilizokuwa ndefu zaidi,”* akasema mwangalizi mkuu wa EU wakati alipokuwa akiwasilisha ripoti ya mwanzo hapo Nairobi. *“Wakenya walisimama kutetea amani na haki zao hapo Jumatatu. Kujitolea kwao kutekeleza haki zao ni mfano mwema si kwa eneo hili tu bali hata ulimwengu mzima.”*

Ilikuwa ni shughuli kubwa na iliyoazimia kufaulisha katika muda wa siku moja uchaguzi wa rais, wabunge, maseneta, magavana pamoja na wawakilishi wa wadi mbalimbali kwenye serikali za majimbo. Wapiga kura waliendelea kuamini tume ya IEBC. Hata hivyo, utaratibu wa kufanya maamuzi usio mnyofu ulipelekea tume kuchelewa mara kwa mara kufanya yaliyostahili. Licha ya haya, tume ya IEBC ilifaulu kukabiliana na matatizo ya kiufundi pamoja na yale ya utenda-kazi siku ya kupiga kura na hivyo basi kuhakikisha uadilifu wa upigaji kura ulilindwa.

Kuna mambo fulani yatakayohitaji kuangaliwa kwa makini zaidi katika siku za usoni kuhusu mchakato wa uchaguzi nchini Kenya. Ingawa mfumo uliopo umetenga nafasi kwa makundi fulani, kuhusika kwa wanawake kama wawaniaji viti hakukuwa kwa kuridhisha kamwe. Aidha, kuna baadhi ya jamii na makundi yaliyotengwa na kusahuliwa ambao hawakupata haki ya kupiga kura kutokana na wao kukosa vitambulisho vya kitaifa. Zaidi ya watu milioni tatu walio na umri wa kupiga kura hawakusajiliwa wakati wa usajili wa wapiga kura na kwa hivyo hawakuweza kupiga kura kwenye uchaguzi huu. Kuna hata wawaniaji walioshinda kesi katika mahakama kuu za kushirikishwa katika uchaguzi lakini bado majina yao hayakujipata kwenye karatasi ya kupigia kura.

Huku upigaji kura ukikamilika na hesabu na ujumuishaji matokeo zikiwa zinaendelea, EU EOM itaendelea kuangalia kwa makini awamu zilizobaki kuhusiana na mchakato huu wa uchaguzi. *“Awamu zilizo mbele ya IEBC na Kenya ni muhimu tu kama ilivyo siku ya upigaji kura.”* akasema Bw.Peterle. *“Kwa Ujumla, uwazi na kuaminika kwa Uchaguzi Mkuu unaweza kukadiriwa tu baada ya kujumlishwa kwa kura na kutangazwa kwa matokeo pamoja na kushughulikiwa kwa tetesi zozote zinazoweza kuzuka.”* Ili kuangalia awamu zilizosalia, EU EOM itaendelea kukaa Kenya hadi tamati ya mchakato mzima. Itawasilisha matokeo yake ya mwisho kwenye ripoti kamili takriban miezi miwili baadaye.

Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana na:

Peter Visnovitz, EU EOM Afisa wa Habari

Rununu: +254 (0) 7249 68788, Barua Pepe: peter.visnovitz@eueomkenya.eu